**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# MWONGOZO WA ELIMU YA MPIGA KURA WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA WA MWAKA 2024

**Simu:** +255 26-2962345-8

**Nukushi:** +255 26-2962348

Tovuti: www.inec.go.tz

*Barua pepe: uchaguzi@inec.go.tz*

*Uchaguzi House,*

*Eneo la Uwekezaji Njedengwa,*

*Kitalu D, Kiwanja Na. 4,*

*5 Barabara ya Uchaguzi,*

*S. L. P. 358,*

***41107 DODOMA, TANZANIA***

# YALIYOMO

DIBAJI ..... IV

SURA YA KWANZA ..... 1

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI ..... 1

1.0 UTANGULIZI ..... 1

1.1 Malengo ya Sura ya Kwanza ..... 1

1.2 Historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ..... 1

1.3 Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ..... 2

1.4 Dira, Dhima na Maadili ya Msingi ..... 3

1.4.1 Dira ..... 3

1.4.2 Dhima ..... 3

1.4.3 Maadili ya Msingi ..... 3

1.5 Majukumu ya Tume ..... 3

1.6 Sheria zinazosimamia Uchaguzi Tanzania ..... 4

1.7 Mzunguko wa Uchaguzi ..... 5

1.7.1 Kabla ya Uchaguzi ..... 5

1.7.2 Wakati wa Uchaguzi ..... 5

1.7.3 Baada ya Uchaguzi ..... 6

SURA YA PILI ..... 7

ELIMU YA MPIGA KURA ..... 7

2.0 UTANGULIZI ..... 7

2.1 Malengo ya Sura ya Pili ..... 7

2.2 Mamlaka ya Tume katika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura ..... 7

2.3 Elimu ya Mpiga Kura ..... 8

2.4 Elimu ya Uraia ..... 8

2.5 Ushirikishwaji wa Wadau wa Elimu ya Mpiga Kura ..... 8

2.5.1 Mpiga Kura ..... 9

**2.5.1.1 Wapiga kura wapya** ........ **9**

**2.5.1.2 Wapiga kura wanaoboresha taarifa** ........ **9**

**2.5.1.3 Wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika** ........ **9**

**2.5.2 Vyama vya siasa** ........ **9**

**2.5.3 Taasisi na asasi za kiraia** ........ **10**

**2.5.4 Vyombo vya habari** ........ **12**

**2.5.5 Taasisi mbalimbali** ........ **12**

**2.5.6 Makundi mbalimbali** ........ **12**

**2.6 Njia Zitakazotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura** ........ **12**

**2.7 Zana za Elimu ya Mpiga Kura** ........ **14**

**SURA YA TATU** ........ **16**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA** ........ **16**

**3.0 UTANGULIZI** ........ **16**

**3.1 Malengo ya Sura ya Tatu** ........ **16**

**3.2 Uanzishwaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura** ........ **17**

**3.3 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura** ........ **17**

**3.3.1 Umuhimu wa uboreshaji** ........ **17**

**3.4 Wajibu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura** ........ **18**

**3.5 Wahusika katika Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura** ........ **18**

**3.6 Sifa za Kujiandikisha kuwa Mpiga Kura** ........ **19**

**3.6.1 Raia wa Tanzania ni nani?** ........ **19**

**3.7 Kukosa Sifa za Kuandikishwa kuwa Mpiga Kura** ........ **20**

**3.8 Utaratibu wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Kituoni** ........ **20**

**3.9 Muda wa Uandikishaji Wapiga Kura** ........ **23**

**3.10 Vituo vya Kujiandikisha** ........ **24**

**3.11 Utaratibu wa Kuanzisha Mchakato wa Kuboresha Taarifa kwa Njia ya Mtandao** ........ **24**

**3.12 Fomu Zitakazotumika wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura** ........ **25**

**3.13 Watendaji wa Uandikishaji** ........ **27**

**3.14 Wakala wa Uandikishaji wa Wapiga Kura** ........ **28**

**3.15 Waangalizi wa Uandikishaji** ........ **29**

**3.16 Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura** ........ **29**

**3.17 Kuweka Pingamizi dhidi ya Aliyeandikishwa kwenye Daftari la Awali** ........ **30**

**3.18 Makosa na Adhabu** ........ **30**

## DIBAJI

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikitoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa uboreshaji wa Daftari, umeandaliwa na Tume ili kuwezesha taasisi na asasi zilizopata kibali cha kutoa elimu iliyokusudiwa na Tume.

Mwongozo huu, umefafanua namna ya utoaji wa elimu na mambo muhimu kuhusu mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ikiwa ni pamoja na sifa za kuandikishwa, muda wa uandikishaji, uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura, watendaji wa uandikishaji, wadau wa uandikishaji na njia za utoaji elimu ya mpiga kura.

Lengo la Mwongozo ni kuwaongoza waelimishaji na kuhakikisha kuwa elimu wanayoitoa inakidhi matakwa ya Katiba, sheria, kanuni, miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume. Ni matarajio ya Tume kuwa Mwongozo huu utawawezesha waelimishaji kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uadilifu.

Jaji (Rufaa) Jacobs C. M. Mwambegele

**MWENYEKITI**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## SURA YA KWANZA

## TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

### 1.0 UTANGULIZI

Sura hii inaelezea historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi tangu ilipoanzishwa mwaka 1993, dira, dhima, maadili ya msingi, majukumu ya Tume, sheria zinazosimamia uchaguzi Tanzania, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na mzunguko wa uchaguzi.

### 1.1 Malengo ya Sura ya Kwanza

Mwisho wa sura hii mwelimishaji aweze kuelewa kuhusu: -

(i) historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;
(ii) dira na dhima;
(iii) maadili ya msingi;
(iv) majukumu ya Tume;
(v) sheria zinazosimamia uchaguzi Tanzania; na
(vi) mzunguko wa uchaguzi.

**Mambo muhimu ya kuzingatia:**

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977
- Sheria zinazohusiana na masuala ya uchaguzi
- Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024
- Dira na Dhima
- Maadili ya Msingi
- Majukumu ya Tume

### 1.2 Historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Mwaka 1991, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Ali Hassan Mwinyi aliteua Tume chini ya Uenyekiti wa Hayati Jaji Mkuu Mstaafu Francis Nyalali. Madhumuni ya Tume hiyo ilikuwa ni kukusanya maoni ya wananchi juu ya kuendelea na mfumo wa chama kimoja au kuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Kutokana na ripoti ya Tume hiyo, ibara ya 3(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ilirekebishwa na kufanya Tanzania kuwa Taifa linalofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Vilevile, Sheria ya Vyama vya Siasa, (Na.5 ya 1992) ilitungwa ili kuwezesha usajili wa vyama vya siasa. Pia, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, (Na.1 ya 1985) na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, (Na.4 ya 1979) zilirekebishwa ili kuondokana na mfumo wa chama kimoja na kuruhusu kufanyika kwa Uchaguzi chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Baada ya marekebisho hayo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilianzishwa tarehe 13 Januari, 1993.

Aidha, mwaka 2021 ulifanyika Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulitoka na azimio la kuboresha mfumo wa uchaguzi nchini. Hivyo, tarehe 23 Desemba 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliunda kikosi kazi cha kutathmini hali ya demokrasia ili kutoa mapendekezo ya kuboresha masuala ya demokrasia na hali ya kisiasa nchini.

Kikosi kazi, kilitoa mapendekezo ya kufanyika kwa maboresho ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Maboresho hayo yalisababisha kutungwa kwa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na.2 ya Mwaka 2024 na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024. Kufuatia kutungwa kwa Sheria hizo, jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi lilibadilika na kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

### 1.3 Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 74(7) na (11) ya Katiba na kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na.2 ya Mwaka 2024, Tume ni idara huru inayojitegemea na inafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao. Katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, Tume haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa.

### 1.4 Dira, Dhima na Maadili ya Msingi

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaongozwa na Dira na Dhima pamoja na Maadili ya Msingi.

#### 1.4.1 Dira

Uwepo wa mfumo wa uchaguzi unaoaminika na unaohakikisha chaguzi huru na haki.

#### 1.4.2 Dhima

Kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi kwa kuzingatia sheria ili kuimarisha demokrasia kwa manufaa ya wananchi, vyama vya siasa na wagombea.

#### 1.4.3 Maadili ya Msingi

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume inazingatia maadili ya msingi yafuatayo: -

(i) uwajibikaji;

(ii) uadilifu;

(iii) ushirikishwaji;

(iv) uwazi;

(v) kutopendelea; na

(vi) weledi.

### 1.5 Majukumu ya Tume

Majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi yameainishwa katika ibara ya 74(6) na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 zikisomwa pamoja na kifungu cha 10 cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na.2 ya Mwaka 2024. Majukumu hayo ni: -

(i) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano na Madiwani kwa Tanzania Bara;

(ii) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na Uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara;

(iii) kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge;

(iv) kuteua na kuwatangaza Wabunge Wanawake wa Viti Maalum katika Jamhuri ya Muungano na Madiwani Wanawake wa Viti maalum kwa Tanzania Bara;

(v) kuandaa na kusimamia kanuni za maadili ya uchaguzi;

(vi) kutoa elimu ya mpiga kura nchini;

(vii) kuratibu na kusimamia taasisi na asasi zinazotoa elimu ya mpiga kura;

(viii) kualika na kusajili waangalizi wa uchaguzi;

(ix) kuajiri au kuteua watumishi na watendaji wa Tume kwa kadri itakavyohitajika kwa kuzingatia masharti ya sheria ya Utumishi wa Umma na masharti mengine yatakayowekwa na Tume; na

(x) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama yalivyoainishwa kwenye Katiba au sheria nyingine yoyote.

**1.6 Sheria zinazosimamia Uchaguzi Tanzania**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuratibu shughuli za uchaguzi itazingatia: -

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

(ii) Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na.2 ya Mwaka 2024 na kanuni zake; na

(iii) Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 na kanuni zake.

Pamoja na sheria tajwa, wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Tume huzingatia sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;

(ii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;

(iii) Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258;

(iv) Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278;

(v) Sheria ya Uraia, Sura ya 357; na

(vi) Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge pale itakapohitajika.

### 1.7 Mzunguko wa Uchaguzi

Ibara ya 42(2) na 65 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, zinaelekeza kuwa uchaguzi mkuu ufanyike kila baada ya kipindi cha miaka mitano. Tume hutumia utaratibu wa mzunguko wa uchaguzi ambao umegawanya shughuli za uchaguzi katika awamu tatu ambazo ni kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

#### 1.7.1 Kabla ya uchaguzi

Katika awamu hii, shughuli zinazofanyika ni: -

(i) maboresho na marekebisho ya sheria, kanuni na maelekezo;

(ii) uandaaji wa maadili ya uchaguzi;

(iii) uandaaji wa bajeti;

(iv) ununuzi wa vifaa;

(v) uteuzi wa watendaji;

(vi) utoaji wa mafunzo kwa watendaji;

(vii) uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura;

(viii) uandikishaji wa wapiga kura;

(ix) uandaaji wa kalenda ya uchaguzi na mpango wa utekelezaji;

(x) utoaji wa habari na elimu ya mpiga kura; na

(xi) uhakiki na ugawaji wa majimbo ya uchaguzi.

#### 1.7.2 Wakati wa uchaguzi

Katika awamu hii, shughuli zinazofanyika ni: -

(i) uteuzi wa wagombea;

(ii) usuluhishi wa migogoro ya uchaguzi;

(iii) utoaji wa habari na elimu ya mpiga kura;

(iv) uratibu wa kampeni za uchaguzi;

(v) kusimamia na kuratibu utekelezaji wa maadili;

(vi) usajili wa waangalizi wa uchaguzi;

(vii) uchapishaji wa karatasi za kura;

(viii) mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi;

(ix) usambazaji wa vifaa vya uchaguzi;

(x) upigaji kura;

(xi) kuhesabu kura;

(xii) kujumlisha kura; na

(xiii) kutangaza matokeo.

**1.7.3 Baada ya uchaguzi**

Katika awamu hii, shughuli zinazofanyika ni: -

(i) tathmini ya uchaguzi mkuu;

(ii) kuandaa taarifa ya uchaguzi mkuu;

(iii) kuandaa na kusimamia chaguzi ndogo;

(iv) ukaguzi wa mapato na matumizi ya fedha na uhakiki wa vifaa vilivyotumika katika uchaguzi mkuu;

(v) kuratibu kesi za uchaguzi;

(vi) marekebisho ya sheria za uchaguzi;

(vii) kupitia na kuboresha mipaka ya majimbo ya uchaguzi;

(viii) kupitia na kuboresha mifumo ya uchaguzi;

(ix) kupitia na kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(x) kupitia na kuboresha muundo wa Tume; na

(xi) kuandaa mpango kazi kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaofuata.

**Maswali ya Tafakuri:**

1. Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ni nini?
2. Taja majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.
3. Taja sheria zinazosimamia uchaguzi Tanzania.
4. Taja shughuli ambazo Tume huzifanya kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

## SURA YA PILI

## ELIMU YA MPIGA KURA

### 2.0 UTANGULIZI

Sura hii inaelezea kuhusu mamlaka ya Tume katika kutoa elimu ya mpiga kura, tofauti kati ya elimu ya mpiga kura na elimu ya uraia, ushirikiano wa Tume na wadau katika kutoa elimu ya mpiga kura, njia na zana zinazotumika kutoa elimu ya mpiga kura.

### 2.1 Malengo ya Sura ya Pili

Mwisho wa sura hii mwananchi aweze kuelewa: -

(i) maana ya elimu ya mpiga kura;
(ii) mamlaka ya Tume katika kutoa elimu ya mpiga kura;
(iii) ushirikiano wa Tume na wadau wa uchaguzi;
(iv) njia zinazotumika kutoa elimu ya mpiga kura; na
(v) zana za elimu ya mpiga kura.

| **Mambo muhimu ya kuzingatia:** | |
|---|---|
| (i) | Elimu ya mpiga kura |
| (ii) | Mamlaka ya Tume katika kutoa elimu ya mpiga kura |
| (iii) | Taasisi na asasi za kiraia |
| (iv) | Makundi mbalimbali |
| (v) | Njia zinazotumika kutoa elimu |
| (vi) | Zana za elimu ya mpiga kura |

### 2.2 Mamlaka ya Tume katika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na.2 ya Mwaka 2024 na kanuni ya 21 na 22 ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2024 zimeipa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi mamlaka ya kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi zinazotoa elimu hiyo. Jukumu hili limekuwa likitekelezwa na Tume kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa sheria.

### 2.3 Elimu ya Mpiga Kura

Elimu ya mpiga kura ni elimu ambayo hutolewa kwa wananchi kwa lengo la kuwawezesha kuelewa taratibu za mchakato wa uboreshaji, wajibu wao na umuhimu wa kushiriki katika zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Vilevile, ni elimu isiyokuwa na hisia, ubaguzi wala itikadi za kisiasa, kidini au kikabila katika mchakato wa uboreshaji wa Daftari.

Elimu hiyo hujibu maswali ya msingi ya mwananchi kama vile nani mwenye sifa ya kuandikishwa, wapi atajiandikisha au ataboresha taarifa zake, utaratibu wa kuboresha kwa njia ya mtandao ukoje, lini, muda gani, atarajie nini akifika katika kituo cha kujiandikisha, nani anapaswa kutoa taarifa za mpiga kura aliyepoteza sifa za kuwa kwenye Daftari na kwa nini mpiga kura atunze kadi yake. Elimu inapomfikia mwananchi kwa usahihi na kwa wakati inamuwezesha kuelewa utaratibu wa uboreshaji na hivyo kumfanya ashiriki vyema kwenye uboreshaji wa Daftari.

### 2.4 Elimu ya Uraia

Elimu ya uraia inahusu haki na wajibu wa raia katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Elimu hiyo humjengea uwezo mwananchi kujitambua na kuzijua haki zake zinazomuwezesha kufanya maamuzi sahihi. Wakati wa uboreshaji wa Daftari, elimu ya uraia inamsaidia mwananchi kujua wajibu wake, haki yake, nafasi yake na umuhimu wa yeye kushiriki katika zoezi hilo.

Elimu ya uraia ni tofauti na elimu ya mpiga kura ambayo inamuwezesha mwananchi kujua sifa za kuandikishwa kwenye Daftari, kujua wapi, lini na muda wa kujiandikisha au kuboresha taarifa na kujua taratibu zinazotakiwa kufuatwa anapokuwa katika kituo cha kujiandikisha.

### 2.5 Ushirikishwaji wa Wadau wa Elimu ya Mpiga Kura

Wadau wa elimu ya mpiga kura ni watu au taasisi ambazo kwa namna moja au nyingine zina mchango katika kufanikisha uboreshaji wa Daftari. Tume imekuwa ikishirikisha wadau mbalimbali wakati wa uboreshaji wa Daftari katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata elimu itakayomuwezesha kuzifahamu taratibu za uboreshaji ili aweze kushiriki vyema kwenye zoezi hilo.

Wakati wa uboreshaji wa Daftari, Tume inashirikisha wadau mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na wapiga kura, vyama vya siasa, taasisi na asasi za kiraia, vyombo vya

habari, maafisa habari wa halmashauri, waangalizi wa ndani wa uboreshaji, taasisi za dini, makundi mbalimbali kama vijana, wanawake, jamii za wafugaji, wavuvi, waokota matunda na wawindaji, watu wenye ulemavu, wasiojua kusoma na kuandika na wazee wa kimila.

#### 2.5.1 Mpiga kura

Mpiga kura ni mtu aliyeandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mujibu wa kifungu cha 81(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 5(1) ikisomwa pamoja na kifungu cha 9 cha Sheria hii, ili mtu aandikishwe kuwa mpiga kura ni lazima awe raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 au ambaye atatimiza umri wa miaka 18 ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu.

##### 2.5.1.1 Wapiga kura wapya

Kundi hili, kwa mujibu wa kifungu cha 9(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, linajumuisha raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 au zaidi na ambao watatimiza miaka 18 ifikapo tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na hawajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria.

##### 2.5.1.2 Wapiga kura wanaoboresha taarifa

Kundi hili linajumuisha wapiga kura waliopo kwenye Daftari wanaohitaji kubadili taarifa, waliohama kata au jimbo na wanaohitaji kurekebisha taarifa zao wakati wa uboreshaji.

##### 2.5.1.3 Wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika

Kundi hili linajumuisha wapiga kura waliopoteza kadi na ambao kadi zao zimeharibika. Wapiga kura hao wanatakiwa kufika kituoni ili kupatiwa kadi mpya.

#### 2.5.2 Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa ni wadau muhimu katika zoezi la uboreshaji wa Daftari. Tume hufanya mikutano na viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajili kamili ili kuwapa taarifa kuhusu uboreshaji wa Daftari na kupata maoni yao. Vyama hivyo vina wajibu wa kuwaelimisha na kuwahamasisha wanachama wao, wafuasi, mashabiki na wananchi kujitokeza kushiriki wakati wa uboreshaji wa Daftari.

### 2.5.3 Taasisi na asasi za kiraia

Taasisi na asasi za kiraia ni wadau muhimu katika mchakato wa uchaguzi, Tume imekuwa ikiwashirikisha katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi kwa kuwa wana uwakilishi katika sehemu kubwa ya jamii. Wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari, wadau hawa hupewa mafunzo na kupatiwa Mwongozo unaotumika kutoa elimu ya mpiga kura ili wapate uelewa wa taratibu na miongozo itakayotumika.

Tume hutoa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu hiyo kwa kuzingatia vigezo, nakala muhimu zinazoambatishwa wakati wa maombi, taarifa za rasilimali watu na ratiba ya utekelezaji wa jukumu hilo: -

**(i) Vigezo vinavyotumika**

Ili taasisi na asasi za kiraia ziweze kupata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo: -

a. iwe imesajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania;

b. iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;

c. ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu watatu, wawili wawe Watanzania;

d. katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;

e. iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

f. iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

**(ii) Viambatisho muhimu**

Taasisi na asasi za kiraia zinapowasilisha maombi kupitia Mfumo wa Usajili wa Waangalizi wa Uchaguzi, Waandishi wa Habari na Asasi za Kiraia zinatakiwa kuambatisha nakala zifuatazo: -

a. nakala au kivuli cha cheti cha usajili;

b. nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi ya kiraia;

c. majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi ya kiraia; na

d. anwani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake.

**(iii) Taarifa za watendaji wa taasisi au asasi na ratiba ya utekelezaji**

Baada ya kupata kibali cha kutoa elimu hiyo taasisi na asasi zitatakiwa kuwasilisha Tume: -

a. taarifa za rasilimali watu watakaotoa elimu ya mpiga kura; na

b. ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa na taasisi au asasi katika halmashauri husika.

**(iv) Tamko la kutekeleza mwongozo wa elimu ya mpiga kura**

a. taasisi au asasi ya kiraia iliyopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura itatakiwa kutoa tamko la kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na maelekezo ya Tume wakati wa kutoa elimu hiyo; na

b. taasisi au asasi ya kiraia iliyopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura itapewa nakala ya Mwongozo huu.

Aidha, katika kuhakikisha kwamba elimu ya mpiga kura inayotolewa na taasisi na asasi za kiraia ndiyo iliyokusudiwa, Tume hufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utoaji wa elimu hiyo.

> *Angalizo*:
>
> **Masharti yanayopaswa kufuatwa na taasisi au asasi wakati wa kutekeleza utoaji wa elimu ya mpiga kura**
>
> Mara baada ya kupata kibali, taasisi au asasi itapaswa kufuata yafuatayo; -
>
> (a) kuzingatia sheria za Tanzania wakati wote wa utoaji wa elimu ya mpiga kura;
>
> (b) kutoa elimu ya mpiga kura katika maeneo iliyoomba;
>
> (c) kuufuata Mwongozo huu na maelekezo mengine yanayotolewa na Tume;
>
> (d) kufuata ratiba ya utoaji wa elimu ya mpiga kura kama ilivyowasilisha;
>
> (e) kuhakikisha zana na nyenzo zitakazotumika zinaakisi maudhui yaliyomo katika Mwongozo; na
>
> (f) kuhakikisha inatoa elimu ya mpiga kura iliyokusudiwa na Tume.

### 2.5.4 Vyombo vya habari

Vyombo vya habari ni miongoni mwa wadau muhimu wa uchaguzi. Vyombo hivi hutumika kama njia ya mawasiliano katika kutoa elimu kwa umma kwa usahihi bila kuwa na mwelekeo wala itikadi za kisiasa, kikanda, kidini au kikabila. Miongoni mwa vyombo hivyo ni magazeti, redio na televisheni.

Tume imekuwa ikiwashirikisha wadau hawa katika kutoa elimu ya mpiga kura kupitia njia mbalimbali zikiwemo vipindi vya redio na televisheni, usambazaji wa habari na taarifa kwa umma, taarifa kwa vyombo vya habari na makala za magazeti.

Katika kuhakikisha kuwa elimu hiyo inatolewa kwa usahihi, Tume hufanya mikutano na wanahabari na kuwaelimisha kuhusu taratibu na miongozo ya uboreshaji wa Daftari.

### 2.5.5 Taasisi mbalimbali

Taasisi mbalimbali zikiwemo za elimu na dini ni miongoni mwa wadau muhimu katika mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.Taasisi hizi zimekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha wananchi kushiriki katika mazoezi ya mchakato wa uchaguzi. Pia, hushirikishwa kwa kupatiwa elimu kuhusu utaratibu unaopaswa kufuatwa wakati wa uboreshaji wa Daftari, ili ziendelee kuwahamasisha wananchi na wapiga kura kushiriki zoezi la uboreshaji.

### 2.5.6 Makundi mbalimbali

Tume inatambua umuhimu na ushiriki wa makundi mbalimbali katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Makundi hayo yanahusisha watu wenye ulemavu, wanawake, vijana, wasiojua kusoma na kuandika, wavuvi, wafugaji, jamii ya wawindaji na waokota matunda. Hivyo, Tume imekuwa ikiyafikia makundi hayo kupitia wawakilishi, ili wawe sehemu ya elimu kuhusu uboreshaji wa Daftari na kuwahamasisha kushiriki katika mchakato huo.

## 2.6 Njia zitakazotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Tume imekuwa na utaratibu wa kuwafikia wapiga kura ili kuwaelimisha kuhusu taratibu mbalimbali za uboreshaji wa Daftari. Katika kutekeleza jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura njia zifuatazo zitatumika: -

(i) **Mikusanyiko ya watu**

Tume imekuwa ikitoa elimu ya mpiga kura kwa kukutana na wadau ana kwa ana kwa kushiriki na kudhamini maonesho na matamasha mbalimbali ikiwemo Sabasaba, Nane Nane, Wiki ya Vijana, Wiki ya Sheria na Wiki ya Mapinduzi**.** Pia elimu hutolewa kwenye masoko, gulio na minada.

(ii) **Mikutano na wadau**

Tume inaratibu mikutano ya wadau wa uchaguzi ngazi ya kitaifa na mkoa kabla ya uboreshaji ili kuwashirikisha kuhusu mchakato wa uboreshaji na kuwahamasisha kushiriki katika mchakato huo. Wadau ambao hushiriki katika mikutano hiyo ni viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa, wawakilishi wa wanawake, vyombo vya habari, wawakilishi wa vijana, wawakilishi wa watu wenye ulemavu, wazee wa kimila na watu wenye ushawishi.

(iii) **Vyombo vya habari**

Tume hutumia vyombo vya habari kufikisha elimu ya mpiga kura kwa wadau wake. Vyombo hivyo ni: -

(a) **Magazeti**

Tume huandaa makala mbalimbali zenye kuhabarisha na kuelimisha kuhusu taratibu na miongozo ya uboreshaji wa Daftari ambayo huchapishwa katika magazeti. Pia, Tume hutoa taarifa kwa umma kuhusu uboreshaji kupitia magazeti.

(b) **Redio na televisheni**

Tume hushiriki katika vipindi mbalimbali vya redio na televisheni kuwaelimisha wananchi kuhusu taratibu na miongozo ya uboreshaji wa Daftari kwa lengo la kuwahamasisha kushiriki katika uboreshaji.

**(c) Mitandao ya kijamii**

Tume inatoa elimu ya mpiga kura kwa kupitia kurasa za Tume kwenye mitandao ya kijamii ikiwemo Instagram, Threads, X (Twitter), Facebook na YouTube ili iweze kuwaelimisha wananchi hususan vijana kuhusu uboreshaji wa Daftari.

**(d) Tovuti**

Tume inatoa elimu ya mpiga kura kwa kutumia tovuti yake (*www.inec.go.tz*) ili kuwaelimisha wananchi na wadau mbalimbali kuhusu uboreshaji wa Daftari.

(iv) **Taasisi na asasi za kiraia**

Tume inazishirikisha taasisi na asasi za kiraia kutoa elimu ya mpiga kura katika uboreshaji wa Daftari. Taasisi na asasi hizo hupatiwa mafunzo na mwongozo wa elimu ya mpiga kura ili kuzijengea uwezo wa kutoa elimu iliyokusudiwa na Tume.

(v) **Machapisho**

Tume huandaa na kugawa machapisho mbalimbali yenye ujumbe kuhusu uboreshaji wa Daftari. Machapisho hayo ni pamoja na vijitabu, majarida na vipeperushi.

(vi) **Sanaa**

Tume hutumia sanaa kutoa elimu ya mpiga kura kuwalenga vijana na watu wasiojua kusoma. Kazi za sanaa ambazo Tume hutumia ni pamoja na nyimbo, maigizo, ngonjera, ngoma na vikaragosi. Kazi hizo huwasilishwa kwa njia ya ana kwa ana au kwa kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

(vii) **Gari la elimu ya mpiga kura**

Tume hutumia gari la elimu ya mpiga kura ambalo hupita katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu na kutoa elimu ya mpiga kura kuhusu uboreshaji wa Daftari. Maeneo ya mikusanyiko ni pamoja na sokoni, minadani, vituo vya mabasi, magulio na shuleni.

### 2.7 Zana za Elimu ya Mpiga Kura

Katika kutoa elimu ya mpiga kura kuhusu uboreshaji, Tume hutumia zana zifuatazo: -

(i) vijitabu vya elimu ya mpiga kura;
(ii) majarida ya elimu ya mpiga kura;
(iii) vipeperushi vya elimu ya mpiga kura;
(iv) sanaa (nyimbo, maigizo na *jingles*) zenye maudhui ya elimu ya mpiga kura; na

(v) mabango (*banners, billboards, tyre covers* na *stickers*) yenye ujumbe wa elimu ya mpiga kura.

**Maswali ya Tafakuri:**

1. Je, ni nani mwenye mamlaka ya kutoa, kusimamia na kuratibu elimu ya mpiga kura nchini Tanzania?
2. Ni vigezo gani ambavyo vinapaswa kuzingatiwa ili taasisi au asasi ya kiraia iweze kupewa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura?
3. Taja wadau wa elimu ya mpiga kura.
4. Taja njia ambazo zinaweza kutumika wakati wa kutoa elimu ya mpiga kura.

## SURA YA TATU

## UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

### 3.0 UTANGULIZI

Sura hii inaelezea uanzishwaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, uboreshaji wa Daftari, wajibu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa uboreshaji wa Daftari, sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, kukosa sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, muda wa uandikishaji wa wapiga kura na wahusika katika uboreshaji wa Daftari.

Pia, sura hii inaelezea utaratibu wa uboreshaji wa Daftari kituoni, vituo vya kujiandikisha, fomu zinazotumika wakati wa uboreshaji wa Daftari, watendaji wa uandikishaji, mawakala wa uandikishaji, waangalizi wa uandikishaji, kuweka wazi Daftari la Awali na utaratibu wa kuweka pingamizi kwa mpiga kura asiye na sifa aliyeandikishwa kwenye Daftari la Awali.

### 3.1 Malengo ya Sura ya Tatu

Mwisho wa sura hii mwananchi aweze kuelewa: -

(i) uanzishwaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(ii) uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iii) kuweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura; na

(iv) Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**Mambo muhimu ya kuzingatia:**

- Majukumu ya Tume wakati wa uboreshaji
- Kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
- Uandikishaji wa wapiga kura wapya (Fomu Na. 1)
- Uboreshaji wa taarifa za mpiga kura (Fomu Na. 5A)
- Kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa (Fomu Na. 5B)

### 3.2 Uanzishwaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limeanzishwa chini ya ibara ya 5(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024. Kabla ya kuundwa kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, wapiga kura walikuwa wakijiandikisha miezi sita kabla ya uchaguzi na kupewa shahada ya muda ambayo baada ya kukamilika kwa uchaguzi husika, shahada hiyo haikuwa na matumizi. Kwa mara ya kwanza wapiga kura walianza kuandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2004 kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005.

### 3.3 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 16(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024. Tume ina wajibu wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya uchaguzi mkuu uliomalizika na kabla ya siku ya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaofuata.

Uboreshaji wa Daftari ni utaratibu unaohusisha uandikishaji wa wapiga kura wapya wenye sifa, kurekebisha au kubadili taarifa za wapiga kura waliojiandikisha awali, kutoa kadi kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea, zimeharibika au zimefutika na kuhamisha taarifa za wapiga kura kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine. Aidha, wapiga kura waliopoteza sifa wataondolewa kwenye Daftari.

#### 3.3.1 Umuhimu wa uboreshaji

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unalenga mambo muhimu yafuatayo: -

(i) kutoa fursa ya kujiandikisha kwa wananchi waliotimiza umri wa miaka 18 na watakaotimiza umri wa miaka 18 ifikapo tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025;

(ii) kutoa fursa ya kujiandikisha kwa wananchi waliotimiza umri wa miaka 18 na kuendelea ambao hawakuwahi kujiandikisha katika Daftari;

(iii) wapiga kura waliopoteza au kadi zao kuharibika kupatiwa kadi mpya;

(iv) kurekebisha au kubadili taarifa za wapiga kura;

(v) kuhamisha taarifa za wapiga kura kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine;

(vi) kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo kwenye Daftari ka Kudumu la Wapiga Kura mfano, waliofariki;

(vii) kusaidia kupata takwimu sahihi ya wapiga kura; na

(viii) kuisaidia Tume kufahamu mahitaji na vitendea kazi vitakavyotumika kwenye uchaguzi.

**3.4 Wajibu wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura**

Katika kutekeleza wajibu wake, Tume hufanya yafuatayo: -

(i) kukagua na kuhakiki vituo vya uandikishaji;

(ii) kupanga ratiba ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iii) kugawa vifaa vinavyotumika katika uboreshaji wa Daftari;

(iv) kuboresha na kutunza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(v) kuteua waratibu wa uandikishaji wa mikoa, maafisa waandikishaji na maafisa waandikishaji wasaidizi, kuwaajiri watendaji wa vituo vya kuandikisha wapiga kura na kuwapatia mafunzo; na

(vi) kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kusimamia na kuratibu taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo wakati wa uboreshaji wa Daftari.

**3.5 Wahusika katika Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura**

Wanaohusika katika zoezi hili ni: -

(i) raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18;

(ii) raia wa Tanzania wenye miaka 18 na kuendelea ambao hawakuwahi kujiandikisha kwenye Daftari;

(iii) raia wa Tanzania watakaokuwa wametimiza miaka 18 ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu;

(iv) wapiga kura waliojiandikisha awali na wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine;

(v) wapiga kura ambao taarifa zao zilikosewa wakati wa uandikishaji;

(vi) wapiga kura waliopoteza kadi, kuharibika au kufutika; na

(vii) wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo kwenye Daftari.

**3.6 Sifa za Kujiandikisha kuwa Mpiga Kura**

Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 9 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 zimeainisha sifa za mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura ambazo ni: -

(i) raia wa Tanzania;

(ii) ametimiza umri wa miaka 18; na

(iii) awe hajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

**3.6.1 Raia wa Tanzania ni nani?**

Kwa mujibu wa Sheria ya Uraia ya Tanzania, Sura ya 357 Rejeo la Mwaka 2002, Tanzania ina raia wa aina tatu: -

(i) **Uraia wa Tanzania kwa kuzaliwa**

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Uraia ya Tanzania, Sura ya 357 Rejeo la Mwaka 2002, kinaeleza kwamba, mtu yeyote anayefuzu kuwa raia wa Tanzania kwa kuzaliwa ni yule aliyezaliwa nchini Tanzania siku ya Muungano au baada ya Muungano ambaye wakati wa kuzaliwa kwake mmoja wa wazazi wake ni raia wa Tanzania.

(ii) **Uraia wa Tanzania kwa kurithi**

Kifungu cha 6 cha Sheria ya Uraia ya Tanzania, Sura ya 357 Rejeo la Mwaka 2002, kinaeleza kuwa, mtu yeyote aliyezaliwa nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya Muungano au baada ya Muungano atahesabika kuwa raia wa Tanzania kwa kurithi kuanzia tarehe ya kuzaliwa kwake kama siku ya kuzaliwa kwake mama au baba yake ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzaliwa au tajnisi.

(iii) **Uraia wa Tanzania kwa tajnisi au kuandikishwa**

Kwa mujibu wa kifungu cha 8 na 9(1) vya Sheria ya Uraia ya Tanzania, Sura ya 357 Rejeo la Mwaka 2002, mtu yeyote ambaye siyo raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzaliwa au kurithi anaweza kuomba uraia wa Tanzania wa Tajnisi.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Waziri mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya uraia nchini ndiye mwenye mamlaka ya mwisho ya kutoa au kutokutoa uraia wa Tanzania kwa wageni walioomba uraia.

**3.7 Kukosa Sifa za Kuandikishwa Kuwa Mpiga Kura**

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024**,** mtu atakosa sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura kwa sababu zifuatazo: -

(i) si raia wa Tanzania;

(ii) yuko chini ya kiapo cha utii kwa nchi nyingine tofauti na Tanzania;

(iii) amethibitika kuwa hana akili timamu;

(iv) ametiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo au anatumikia kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake inazidi miezi sita iliyotolewa na Mahakama au kama ilivyobadilishwa na mamlaka yenye dhamana;

(v) amezuiliwa kujiandikisha kuwa mpiga kura na sheria za uchaguzi au sheria nyingine kwa makosa yanayohusiana na uchaguzi; na

(vi) hatakuwa ametimiza umri wa kupiga kura, ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu.

**3.8 Utaratibu wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Kituoni**

**i. Uandikishaji wa wapiga kura wapya**

(a) uandikishaji huu utafanyika katika kituo cha kuandikisha wapiga kura;

(b) mwombaji atawasili kituoni na kujipanga kwenye mstari. Kipaumbele kitatolewa kwa wajawazito, akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni, wagonjwa, wazee na watu wenye ulemavu;

(c) mwombaji atajitambulisha kwa mwandishi msaidizi na baada ya kuridhika kuwa ana sifa za kuandikishwa, mwombaji atajaza Fomu Na.1;

(d) mwombaji mpya mwenye kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA, atampatia mwandishi msaidizi kitambulisho chake au namba yake ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa zake kwenye mfumo na kuchukua alama za vidole na picha;

(e) mwombaji ambaye ni raia wa tajnisi ni lazima aoneshe hati ya uraia wa kuandikishwa;

(f) mara baada ya kujaza taarifa zake, mwandishi msaidizi atamwelekeza kwenda kwa mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki kwa ajili ya kuingiza taarifa za mwombaji kwenye BVR kit; na

(g) baada ya uandikishaji kukamilika atapewa kadi.

**ii. Mpiga kura anayetaka kuboresha taarifa zake**

(a) mpiga kura ambaye anataka kurekebisha au kuhamisha taarifa zake anatakiwa kufika katika kituo cha uandikishaji akiwa na kadi ya mpiga kura. Kadi hiyo itasaidia kupata taarifa zake ili kuwezesha uboreshaji kufanyika kwa haraka katika mfumo;

(b) mpiga kura atajaza Fomu Na. 5A na kuipeleka kwa mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki;

(c) mpiga kura ambaye hatakuwa na kadi yake ya awali taarifa zake zitatafutwa kwenye mfumo. Endapo taarifa zake hazitapatikana, mpiga kura ataandikishwa upya kwa kutumia Fomu Na.1 na zoezi la uchukuaji alama za vidole, picha na saini litaendelea; na

(d) mpiga kura aliyepoteza au kadi yake kuharibika atajaza Fomu Na. 5A na kuipeleka kwa mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki kisha atapatiwa kadi mpya.

**iii. Mpiga kura aliyepoteza kadi au kadi yake kuharibika**

Mpiga kura aliyepoteza kadi au kadi yake kuharibika atafika kituoni na kutaja majina yake (matatu) kama alivyojiandikisha awali au namba ya kadi ya mpiga kura au namba ya simu aliyoitumia kujiandikisha awali. Mwombaji atajitambulisha kwa mwandishi msaidizi na baada ya kuridhika kuwa ana sifa atampatia Fomu Na. 5A ili aijaze.

Mwandishi msaidizi atamwelekeza mwombaji kwenda kwa mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki kwa ajili ya kuingiza taarifa zake kwenye mfumo wa

kuandikisha wapiga kura kisha, mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki atajaza taarifa kwenye mfumo na atampatia kadi ya mpiga kura.

**iv. Kukataliwa kuandikishwa kuwa mpiga kura**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 na kanuni ya 23 ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, mwandishi msaidizi asiporidhika kuwa mwombaji ana sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura anaweza kukataa kumwandikisha. Baada ya kukataa kumwandikisha na endapo mwombaji atahitaji kuandikishwa, hatua zifuatazo zitachukuliwa: -

(a) afisa mwandikishaji atamtaarifu mwombaji sababu za kutomwandikisha kwa kujaza nakala mbili za Fomu Na. 3A;

(b) mwombaji ambaye hataridhika na uamuzi wa mwandishi msaidizi anaweza kupeleka Fomu Na. 3A kwa afisa mwandikishaji ndani ya siku saba kwa ajili ya mapitio ya uamuzi wa mwandishi msaidizi;

(c) afisa mwandikishaji atatoa uamuzi ndani ya siku 14 katika Fomu Na. 3A kwa kuonesha iwapo mwombaji ana sifa au amekosa sifa za kuandikishwa na kumjulisha mwombaji;

(d) endapo afisa mwandikishaji atakubaliana na uamuzi wa mwandishi msaidizi, mwombaji huyo hataandikishwa;

(e) iwapo afisa mwandikishaji hatakubaliana na uamuzi wa mwandishi msaidizi, ataandika uamuzi wake katika Fomu Na. 3A na atamwelekeza mwombaji huyo kurudi kwenye kituo ili akajiandikishe; na

(f) mwombaji ambaye hakuridhika na uamuzi wa kutokuandikishwa na afisa mwandikishaji, anaweza kukata rufaa ndani ya siku 14 katika Mahakama ya Mwanzo na uamuzi wa mahakama utakuwa ni wa mwisho.

Endapo kipindi cha uandikishaji kitakuwa kimekwisha na mahakama ikaamua kuwa mwombaji huyo anazo sifa za kuandikishwa, afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi atamwandikisha mwombaji huyo kwa mujibu wa sheria.

v. **Mpiga kura aliyepoteza sifa ya kuwemo kwenye daftari**

Mpiga kura aliyepoteza sifa za kuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ataondolewa kwenye daftari kwa kujaza au kujaziwa **Fomu Na. 5B.** Utaratibu wa kumuondoa mpiga kura aliyepoteza sifa ni kama ifuatavyo: -

(a) mtoa taarifa lazima awe amejiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(b) mtoa taarifa anatakiwa kuwa na kadi au namba ya kadi ya mpiga kura ya anayemtolea taarifa; na

(c) mtoa taarifa za mpiga kura aliyefariki atapaswa kutoa tamko la uthibitisho wa kifo cha anayemtolea taarifa.

**3.9 Muda wa Uandikishaji Wapiga Kura**

Kwa mujibu wa kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2024, Tume hupanga muda wa kuandikisha wapiga kura. Uandikishaji wa wapiga kura hufanyika kwenye vituo vya uandikishaji vilivyoanzishwa na kutangazwa na Tume. Mtu mwenye sifa za kuandikishwa ataenda mwenyewe kituoni.

Aidha, vituo vyote vitafunguliwa kuanzia saa mbili kamili (02:00) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12:00) jioni.

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

Ni muhimu mpiga kura: -

- kukagua kadi yake kabla hajaondoka kituoni ili kama kuna makosa ya taarifa zake yaweze kurekebishwa haraka;
- kurudisha kadi iliyoharibika kabla ya kuchapishiwa kadi mpya;
- kuhakikisha anapatiwa kadi mpya;
- kutunza kadi yake mahali salama wakati wote. Kadi hiyo inatumika kwa ajili ya kupigia kura tu; na
- kipaumbele kitatolewa kwa wakina mama wajawazito, wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni, wagonjwa, wazee na watu wenye ulemavu.

### 3.10 Vituo vya Kujiandikisha

Kila kijiji au mtaa kutakuwa na angalau kituo kimoja cha kuandikisha wapiga kura na kwa upande wa mamlaka ya miji midogo kutakuwa na angalau kituo kimoja katika baadhi ya vitongoji. Vituo vya kuandikisha wapiga kura vimepangwa katika majengo ya umma au maeneo ya wazi yanayofikika kwa urahisi. Orodha ya vituo itakabidhiwa kwa vyama vya siasa mapema kabla ya uboreshaji kuanza.

> ***Angalizo***
>
> Maeneo yafuatayo hayaruhusiwi kuwa na vituo vya kuandikisha wapiga kura; kambi za jeshi, vituo na kambi za polisi, sehemu za kuabudu kama kanisani na msikitini na majengo au ofisi za vyama vya siasa.

### 3.11 Utaratibu wa Kuanzisha Mchakato wa Kuboresha Taarifa kwa Njia ya Mtandao

Utaratibu huu unamlenga mpiga kura aliyeandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura anayehitaji kurekebisha au kubadilisha taarifa zake, kuhamisha taarifa zake kutoka kituo cha awali kwenda kingine au anayetaka kufanya vyote kwa pamoja. Katika kutekeleza mchakato huo, mpiga kura anatakiwa kufuata hatua zifuatazo: -

i. Ataingia kwenye tovuti ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi *www.inec.go.tz* kwa kutumia kompyuta au simu janja kisha atabonyeza kiunganishi (link) kilichoandikwa "**Boresha Taarifa za Mpiga Kura**" au atatumia anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** itakayompeleka moja kwa moja kuanzisha mchakato. Baada ya kufuata utaratibu huo, mfumo utamletea ukurasa wenye vipengele vitatu kama inavyooneshwa kwenye picha ifuatayo: -




ii. Baada ya kumaliza mchakato mmojawapo kati ya iliyoainishwa kwenye picha, mfumo utamjulisha mpiga kura papo hapo kuwa ombi lake limepokelewa; na

iii. Baada ya ombi hilo kufanyiwa kazi na Tume, mpiga kura atapokea ujumbe mfupi wenye kumbukumbu namba kupitia namba yake ya simu aliyoitumia kuboresha taarifa zake kwenye mfumo. Kumbukumbu namba hiyo atakwenda nayo kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura kwa ajili ya kumalizia hatua zilizobaki na kupatiwa kadi.

***Angalizo*:**

Mpiga kura aliyepoteza kadi au kadi yake kuharibika hatahusika na utaratibu huu, hivyo atalazimika kufika kituo cha kuandikisha wapiga kura na kufuata taratibu zote zilizowekwa.

**3.12 Fomu zitakazotumika Wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura**

Tume hutumia fomu zifuatazo wakati wa uboreshaji wa Daftari: -

(i) **Fomu Na. 1**

Fomu hii hutumika kuandikisha wapiga kura wapya.

(ii) **Fomu Na. 5A**

Fomu hii hutumika kufanya masahihisho ya taarifa za mpiga kura zilizokosewa awali, uhamisho wa taarifa za mpiga kura ambaye amehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda lingine kutoa tamko la kupotea au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura.

(iii) **Fomu Na. 5B**

Fomu hii hutumika kufuta taarifa za mpiga kura aliyekosa au kupoteza sifa za kuwa kwenye Daftari wakiwemo wapiga kura waliofariki.

(iv) **Fomu Na. 2**

Fomu hii hutumika kujaza idadi ya fomu zilizotumika na zilizo haribika kwa siku husika katika kituo cha uandikishaji

(v) **Fomu Na. 3A**

Fomu hii hutumiwa na mwandishi msaidizi kuonesha kutokubali ombi la kujiandikisha mtu asiye na sifa kwa kuainisha sababu ya kufanya hivyo.

(vi) **Fomu Na. 3B**

Fomu hii hutumika kupinga kuendelea kuwepo kwa jina lolote la mpiga kura aliyekosa sifa ya kuwemo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Fomu hii hujazwa wakati wa uwekaji wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura.

(vii) **Fomu Na. 6**

Fomu hii hutumika kwa ajili ya kutoa tamko la kujitoa uanachama au kutokuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa.

(viii) **Fomu Na. 7**

Fomu hii hutumika kwa ajili ya kiapo cha kutunza siri kwa watendaji wa uandikishaji na mawakala wa uandikishaji.

(ix) **Fomu Na. 4**

Fomu hii ni ya mkataba wa ajira kwa waandishi wasaidizi na waendeshaji wa vifaa vya bayometriki.

***Angalizo*****:** Fomu Na. 4, 6 na 7 hazitumiki kwenye kituo cha uandikishaji.

**3.13 Watendaji wa Uandikishaji**

Kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 7(1),9(1) na 11(1) za Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi hutumia watendaji mbalimbali wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Watendaji hao ni pamoja na: -

(i) **Mratibu wa uandikishaji wa mkoa**

Ni mtendaji aliyeteuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi miongoni mwa watumishi wa umma kusaidia kuratibu masuala ya uboreshaji wa Daftari katika mkoa husika.

(ii) **Afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi**

Ni mtendaji aliyeteuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi miongoni mwa watumishi wa umma kusimamia shughuli za uboreshaji wa Daftari katika halmashauri.

(iii) **Mwandishi msaidizi**

Ni mtendaji aliyeteuliwa na afisa mwandikishaji kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura katika kituo cha uandikishaji ambaye pia ni kiongozi wa kituo cha uandikishaji wa wapiga kura. Iwapo kutakuwa na mwandishi msaidizi zaidi ya mmoja kwenye kituo, afisa mwandikishaji atateua kiongozi kutoka miongoni mwa waandishi wasaidizi.

(iv) **Mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki**

Ni mtendaji aliyeteuliwa na afisa mwandikishaji kuingiza taarifa za wapiga kura katika mfumo wa kuandikisha wapiga kura kwa kutumia *BVR Kit.*

### 3.14 Wakala wa uandikishaji wa wapiga kura

Ni mtu aliyeteuliwa na chama cha siasa chenye usajili kamili kuwepo kwenye kituo cha uandikishaji kwa lengo la kuwatambua watu wenye sifa za kuandikishwa na kuona iwapo taratibu za uboreshaji wa Daftari zinafuatwa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, kila chama cha siasa chenye usajili kamili kinaweza kumteua mtu mmoja kuwa wakala wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari kwa kila kituo cha uandikishaji.

**(i) Wajibu au majukumu ya wakala wa uandikishaji**

Mawakala wa uandikishaji watatekeleza majukumu yafuatayo: -

(a) kufuatilia zoezi la uboreshaji na kumsaidia mwandishi msaidizi kutekeleza ipasavyo sheria na taratibu zinazohusu mwenendo wa uandikishaji wa wapiga kura bila kuingilia majukumu yake; na

(b) kushirikiana na waandishi wasaidizi kutambua watu wenye sifa za kuandikishwa wakiwemo wakazi wa eneo husika.

Pamoja na majukumu tajwa, mawakala wa uandikishaji hawataruhusiwa kufanya yafuatayo;

(a) kuingilia shughuli za uboreshaji kituoni;

(b) kufanya kampeni za kisiasa katika kituo cha uandikishaji; na

(c) kuorodhesha majina ya watu wanaojiandikisha.

**(ii) Kiapo cha kutunza siri cha wakala wa uandikishaji**

Kila wakala wa uandikishaji kabla ya kuanza kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ni lazima aape kiapo cha kutunza siri za taarifa za mwombaji aliyeomba kuandikishwa au mpiga kura anayeboresha taarifa zake. Wakala ataapa kiapo kwa kujaza Fomu Na. 7 mbele ya afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi siku saba kabla ya kuanza uboreshaji.

> ***Angalizo*:**
>
> Kutokuwepo kwa wakala kituoni hakutazuia au hakutabatilisha jambo ambalo limefanyika kwa mujibu wa sheria na haitachukuliwa kuwa ni kinyume cha sheria iwapo jambo hilo au hatua hiyo itafanyika bila wakala wa uandikishaji kuwepo.

### 3.15 Waangalizi wa Uandikishaji

Kwa mujibu wa kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, waangalizi wa ndani na wa kimataifa wanaruhusiwa kutazama mchakato wa uboreshaji utakavyofanyika katika vituo vya uandikishaji.

Kwa kuzingatia kanuni ya 46(3) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, waangalizi wa uboreshaji wanapaswa kuomba kibali cha kutazama uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Tume baada ya kupokea maombi inaweza kukubali au kukataa maombi hayo.

Waangalizi ambao maombi yao yamekubaliwa watapewa barua na Tume za kuwatambulisha kwa maafisa waandikishaji. Aidha, maafisa waandikishaji watatakiwa kuwapatia barua za kuwatambulisha kwa watendaji wa vituo ambavyo watavitembelea.

> ***Angalizo:***
>
> Waangalizi hawaruhusiwi kuingilia mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika kituo husika. Aidha, watatakiwa kuzingatia Mwongozo wa Waangalizi wa Uandikishaji ulioandaliwa na Tume.

### 3.16 Uwekaji Wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, Tume inatakiwa kuweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura ili kutoa fursa ya: -

(i) kuhakiki usahihi wa taarifa;

(ii) kuboresha taarifa iwapo zimekosewa; na

(iii) kuweka pingamizi kwa mpiga kura aliyepoteza sifa.

**Njia zinazotumika kuhakiki taarifa za mpiga kura ni: -**

(i) kufika katika kituo cha kuandikisha wapiga kura na kukagua taarifa;

(ii) kutumia tovuti ya Tume (www.inec.go.tz);

(iii) kuhakiki taarifa kwa kutumia mfumo wa uhakiki wa wapiga kura (Voter Interaction System -VIS) kupitia kiunganishi cha *vis.inec.go.tz ;*

(iv) kupiga Na.*152*00# (bure) kwa kutumia simu ya mkononi na kufuata maelekezo; na

(v) Kupiga Na. 0800112100 (bure) ya huduma kwa mpiga kura na kuongea na watumishi wa Tume.

### 3.17 Kuweka Pingamizi dhidi ya Aliyeandikishwa kwenye Daftari la Awali

Kifungu cha 27 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 na kanuni ya 37 ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, zimeweka utaratibu wa uwasilishaji wa pingamizi wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura kama ifuatavyo:-

(a) pingamizi linaweza kuwekwa na mtu yeyote aliyeandikishwa katika Daftari;

(b) pingamizi linatakiwa liwasilishwe kwa afisa mwandikishaji ndani ya siku saba kuanzia siku ya mwisho ya uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura;

(c) pingamizi litawasilishwa kwa kujaza nakala mbili za Fomu Na. 3B;

(d) afisa mwandikishaji baada ya kupokea pingamizi atamtaarifu mhusika sababu za kuwekewa pingamizi ndani ya siku saba na kumtaka atoe maelezo ya utetezi wake kwa maandishi;

(e) afisa mwandikishaji atatoa notisi ya siku saba kuwajulisha mahali, tarehe na muda atakaosikiliza pingamizi hilo; na

(f) afisa mwandikishaji atafanya uamuzi wa kukubali au kukataa pingamizi na kuwajulisha wahusika juu ya uamuzi aliofanya.

### 3.18 Makosa na Adhabu

Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 imeainisha makosa mbalimbali yanayofanywa na watendaji wa uboreshaji na wadau wa uchaguzi pamoja na adhabu kuhusiana na makosa hayo.

(i) **Afisa Mwandikishaji**

Kifungu cha 120(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, kinaeleza kuwa ni kosa kwa afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi kuvuruga mchakato wa uandikishaji kwa makusudi. Endapo atapatikana na hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano **(500,000/=)** na isiyozidi shilingi milioni moja **(1,000,000/=)** au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

(ii) **Mwandishi Msaidizi na Mwendeshaji wa Vifaa vya Bayometriki**

Kwa mujibu wa kifungu cha 120(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, ni kosa kwa mwandishi msaidizi au mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki kuvuruga mchakato wa uandikishaji kwa makusudi. Endapo atapatikana na hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili **(200,000/=)** na isiyozidi shilingi laki tano **(500,000/=)** au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

(iii) **Mwombaji au Mpiga Kura**

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, mtu yeyote anayeomba kuandikishwa atakuwa ametenda kosa ikiwa atafanya yafuatayo: -

(a) kutoa taarifa za uongo dhidi yake au mtu mwingine ili aandikishwe kuwa mpiga kura;

(b) kulaghai kuandikishwa bila kuzingatia kifungu cha 25 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024;

(c) kuomba kuandikishwa zaidi ya mara moja;

(d) kuomba kupatiwa kadi nyingine ya mpiga kura bila kuwa na sababu zinazoruhusiwa kisheria;

(e) kutoa tamko la uongo; au

(f) kununua, kuuza, kuiba, kufuta au kuharibu kadi ya mpiga kura.

Mtu yeyote akitiwa hatiani kwa kosa lolote kati ya hayo atapewa adhabu ya kulipa faini isiyopungua kiasi cha shilingi laki moja **(100,000/=)** na isiyozidi shilingi laki tatu **(300,000/=)** au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 114(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, ni kosa kwa mpiga kura ambaye jina lake limefutwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kukataa kurudisha kadi ya mpiga kura. Mtu yeyote akitiwa hatiani kwa kosa hilo atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini **(50,000/=)** na isiyozidi shilingi laki moja **(100,000/=).**

**Maswali ya Tafakuri:**

1. Kwa nini Tume hufanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura?
2. Taja sifa za mtu kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
3. Taja sababu zinazomkosesha mtu sifa za kujiandikisha kuwa mpiga kura.
4. Taja wahusika katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
5. Kwa nini Tume huweka wazi Daftari la awali?
6. Taja majukumu ya mwendeshaji wa vifaa vya bayometriki.
7. Taja wajibu na majukumu ya wakala wa uandikishaji.
8. Taja makosa yanayoweza kufanywa katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**Email**: uchaguzi@inec.go.tz, info@inec.go.tz

**Tovuti**: https://www.inec.go.tz/

**INEC online TV:** https://www.youtube.com/@inectzonlinetv

**X (Twitter)**: https://twitter.com/TumeUchaguziTZ

Instagram **Instagram**: https://www.instagram.com/tumeyauchaguzi_tanzania

**Instagram threads:** https://www.threads.net/@tumeyauchaguzi_tanzania

**Facebook**: **TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

Channels **WhatsApp Channel: TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**